salsa
small farms
small food businesses and
sustainable food security

Muktasari wa sera-mafunzo kutoka Afika

Machi 2020

Tatizo kuu ya mifumo ya chakula ya Afrika ni kutoa chakula kwa idadi ya watu wanaokua ambao wanapenda aina tofauti ya vyakula. Huku idadi ya watu katika bara la Uropa ikipungua na wazalishaji wakitaka vyakula vilivyozalishwa katika njia sawa kimazingira na kisosiolojia, idadi ya watu barani Afrika itaongezeka mara dufu kati ya 2020 na 2050 pia mahitaji yataongezeka kwa sababu ya kubadilika kwa vyakula.

MIKOA YA AFRIKA ILIYOCHAMBULIWA NA SALSA
Santiago Island (CAPE VERDE) - Gushegu (GHANA),
Ugunja (KENYA) - Balaka (MALAWI) - Haouaria (TUNISIA)



Source: UN - adapted by SALSA

SALSA ni mradi wa EU Horison 2020 ambayo inachunguza kazi ya sasa na baadaye ya mashamba madogo na biashara ndogo ndogo inayohusiana nayo (wauzaji, waundaji, na wasambazaji) katika kuafikia maendeleo endelevu ya chakula na usalama wa chakula (FNS). Sehemu moja muhimu ya mradi huu ulikuwa kutambua mazingira ya kuwezesha ya mashamba madogo kuafikia mahitaji yanayozidi kuongezeka ya chakula katika dunia iliyojaa watu na rasilimali kidogo.

SALSA ilichunguza mashamba madogo katika maeneo 30 za inchi 20- maeneo 25 (katika viwango vya kiutawla vya NUTS3) barani Uropa na maeneo 5 barani Afrika. Katika bara la Afrika maeneo rejelewa yalikuwa katika viwango vya mikoa(Ghana na Malawi), gatuzi (Kenya), watu wanaoishi pamoja(Tunisia) ama visiwa (Cape Verde)

Mradi ulilenga mashamba madogo ya viwango vya ekari 5 na kiwango cha kiuchumi cha kufikia 8(sawa na 9,600 ya kiasi jumla cha wastani). Watafiti wa SALSA walitilia maanani uhusiano kati ya mashamba madogo na familia zao cha muhimu kikiwa kujitolea wenyewe.

Katika kila maeneo yaliyofanyiwa utafiti na SALSA,elimu ya mfumo wa chakula ya bidhaa mbili au nne zilichaguliwa. Kwa kutambua sifa za kila mfumo wa chakula kimaeneo kwa aina ya bidhaa zilizochaguliwa mradi wa SALSA: a) iliangazia njia tofauti ambazo mashamba madogo na biashara ndogo ndogo yanaweza kuchangia katika utoaji, kuwepo kwa chakula na upatikanaji wa chakula (vigezo vitatu muhimu vya FNS) katika kulinganisha mifumo ya chakula kimaeneo na b) kueleweka vizuri kwa utendakazi wa jumla wa mifumo hii ya chakula.

VIPI HALI YA MASHAMBA MADOGO BARANI AFRIKA?

Bara la Afrika lina idadi kubwa ya watu wanaozidi kuwa katika karne ya 21. Imekadiriwa kufikia bilioni 2.5 mwaka wa 2050 idadi kubwa ya watu wakikadiriwa kubakia katika maeneo ya mashambani mpaka miaka ya 2040. Ingawa hakuna data iliyotolewa ya nchi zote za Afrika kuhusu idadi ya mashamba, FAO imekadiria mashamba ya ukulima milioni 60 yanayotoa kazi kwa wafanyakazi wakulima milioni 220.

Mashamba madogo katika bara la Afrika yanakadiriwa kufanya asilimia 70 ya kazi za ukulima barani, hivyo kusaidia katika kuhakikisha kazi kwa wakaazi wa mashambani. Data zinazopatikana zinaonyesha kuna shida kubwa sana kuhusiana na kutokuwa na usalama wa chakula na lishe bora. Kuzalisha vyakula vya kutosha katika bara la Afrika kimaendeleo kupitia mazingira sawa kisosiolojia itahitaji maendeleo katika uzalishaji kwamashamba ya aina zote.

Kulingana na watenda kazi wa EU kuhusu eneo za vijijini (2019), asilimia 52 ya wakulima waafrika hulima chini ya ekari moja ya mashamba na asilimia 76 wako na mashamba chini ya ekari 2. Wakulima hawa huwa wakulima wa kifamilia ambao huzalisha chakula kwa kuuza na matumizi ya nyumbani. Wakulima wanaosimamia mashamba madogo hupata shida kufikia masoko kwa hivyo hutumia kiwango kikubwa ya mazao yao- haya ni masuala yanayofanya maeneo ya Afrika yaliyofanyiwa utafiti na miradi ya SALSA kuwa sawa na miradi yaliyofanyiw utafiti katika mashariki ya bara Uropa.

NI NANI WAKULIMA WADOGO KATIKA MAENEO YA SALSA AFRIKA?

Ili kushughulikia miktadha mbalimbali ambazo mashamba madogo yanapatikana katika maeneo yaliyofanyiwa utafiti, SALSA ilitoa novela ya aina za mashamba madogo ya Uropa na Afrika.

Novela hii inahusisha sifa tatu mahususi: 1) kiwango cha mwingiliano kwa soko; 2) matumizi ya vidhibitisho na 3) kiwango cha utegemezi kwa mashirika ya pamoja. Aina hizi inakubalisha utofauti kati ya viwango vya mapato ya mashamba yanayozalishwa na shughuli za kilimo hivyo kuangazia tofauti kati ya mashamba yanayoonekana kulemewa na karibu kuwa maskini kutoka kwa yale yenye utajiri, yenye umaalumu,yenye kupangwa katika mashirika na kuingia katika masoko kwa njia tofauti tofauti.

Katika maeneo rejelewa yalifanyiwa utafiti na SALSA, mashamba madogo yaliyopatikana sana sana yalikuwa 'ya muda' na 'wapambanaji wa kawaida'. Aina hizi mbili hula kiwango kikubwa cha mazao na kuacha asilimia kidogo kuuza kwa wanunuzi wa karibu, masoko ya kimaeneo na wauzaji wa jumla. Kwa sababu hii, hawazingatii soko wakilinganishwa na aina hizo zingine tatu za mashamba madogo yaliyotambuliwa na SALSA. Kuongezea, ni nadran kwa wanaozalisha, wanabiasha wadogo na mashirika ya jumla kupatikana katika mahali pa kuuzia pa mashamba madogo. Jinsi mfumo wa chakula unavyoegemea kuwa maalum na wenye usafirishaji, ndivyo viwango vya mazao ya mashamba madogo yanavyoliwa nyumbani.

Aina za mashamba ya SALSA



1. Mashamba ya Muda

2. Wapambanaji wa kawaida

3. Wajasiriamali wa kawaida

4. Wanaofanya biashara

5. Wafanyabiashara wa kimataifa.

Aina nyingi za mwakilishi barani Afrika

Ukulima unaonekana kuwa wa muda tu na shughuli za ukulima zinasaidia njia zingine za mapato. Ukulima unafanywa na wakulima vijana ambao walianza ukulima kwa hiari yao na mazao yao husalia kuliwa nyumabni.

Hawa ni wakulima maskini na wazee. Ukulima wao ni wa kitamaduni. Ukulima wao ni wa kitamaduni na ndio njia yao kuu ya mapato, matumizi ni ya kinyimbani.

Ni matajiri kiasi, wazee kiasi na wamenawirikatika ukulima. Wao hutegemea wafanyakazi wa familia na hupata soko kupitia mashirika ya pamoja.

Matajiri, wazee kiasi na wamejikita katika ukulima. Wao hutumia wafanyakazi wanaolipwa na wanafikia soko kupitia mashirika ya pamoja na wanawekeza katika udhibitisho.

Matajiri sana ambao ni vijana na wageni katika ukulima. Wao hutumia wafanyakazi wa kulipwa na wana wanunuzi wenye tajriba tofauti tofauti.

Sifa bainifu kati ya wakulima wa muda na wapambanaji wa kawaida ni kwamba wakulima wa muda ni wachanga na wana njia zingine za mapato isipokuwa ukulima. Wapambanaji wa kawaida ni wazee, watamaduni na wana mapato ya chini kwa wote.wanapatika katika maeneo mengi yaliyofanyiwa utafiti na mradi wa SALSA lakini ndio wamesambaa sana katika maeneo ya Afika na Uropa kaskazini.

Asilimia 89 ambayo ni 15 juu ya 17 ya bidhaa ya chakula kwenye mfumo inaonyesha kwamba bidhaa zilizozalishwa zilitumika katika maeneo hivyo kuchangia sana kwa upatikanaji wa chakula katika maeneo hayo. Maeneo mawili tu ya mfumo wa chakula (kutoka kata ya Gushegu nchini Ghana) bidhaa zilisafirishwa nje ya eneo hivyo kuonyesha usawa katika matumizi ya kimaeneo na uingiaji katika masoko.

WAKULIMA WADOGO KATIAK MAENEO YA SALSA WANACHANGIA VIPI KATIKA MFUMO WA CHAKULA KIMAENEO?

Ili kuelewa mchango tofauti ya mashambama madogo kwa mfumo wa chakula kimaeneo, mradi wa SALSA ilitengeneza aina za mifumo ya chakula kimaeneo katika bara la Uropa na Afrika. Hii ilikuwa imeegemea asilimua ya mapato ya mashamba madogo kwa mfumo wa chakula na asilimia ya vyakula vinavyoliwa katika maeneo ama yanayosafirishwa nje.

Aina tatu za chakula zilizopatikana ni 1) maeneo (ambapo kiasi kubwa kinaliwa kimitaa); 2) usafirisha wa nje (ambapo kiasi kikubwa kinasafirishwa nje ya maeneo) 3) usawa (kati ya kimaeneo na usafirishaji).matokeo ya takwimu hizi yanaonyesha kwamba katika meneo yaliyofanyiwa utafiti na SALSA, mashamba madogo huchangia sana katika mfumo wa chakula yakitoa asilimia60-100 ya idadi jumla ya bidhaa muhimu zinazozalishwa katika maeneo,

NI NINI MAHITAJI NA MAZINGIRA YA KUWEZESHA YA MASHAMBA MADOGO KATIKA MAENEO YA SALSA BARANI AFRIKA?

Kwa sababu ya idadi kubwa ya aina za mashamba madogo na ujumuishaji dhaifu katika masoko, wanasera ambao wanataka kutengeneza njia mwafaka kwao wanapaswa kuafikia mambo kama kuhimiza na kuangalia kiwango cha kuitikika katika sera kwa aina lengwa ya wakulima. Hii ni kweli kwa wakulima ‘wapambanaji wa kawaida’ ambao ni wazee huku wale ‘wa muda’ wanaweza kushirikishwa kwa biashara mseto wa vijijini na kutolewa kwa huduma za vijijini ambazo zinaweza kusalia huko.

Huku kukizingatiwa kwamba masoko yasiyo rasmi yataendelea kuwa njia muhimu kwa mashamba madogo, hali moja muhimu ya kuongeza au kiumarisha ujumuishaji wa mashamba madogo katika masoko ya kijamii, kimaeneo na ya usafirishaji wa nje ni uundaji na

© SALSA

uhumizaji wa njia mwafaka za viwango vya usalama wa chakula. Kutilia maanani viwango hivi junahitaji mafuzo na njia zingine za kusaidia(kama pesa za kuwekeza za viwango vidogo) ili kusaidia wakulima kuchukua viwango na kuzalisha vifaa vinavyostahili.

Vyama vya ushirika vilitambuliwa kama viungo muhimu katika mfumo wa chakula kimaeneo na huwezesha mashamba madogo kuongeza mazao yao na kushinda vizingiti vya kimuundo katika viwango. Tahadhari inapaswa kuwekwa kwa mifano yaliyofaulu ya mashamba madogo ili kuongeza/ kuipa nguvu ili iingiliane na mifumo ya kibishara ya kitaifa, kimaeneo na kimataifa.

SALSA ilifanya uchambuzi wa muundo wa mipango ya kilimo ya kitaifa barani Afrika na kuonyesha kwamba, serikali za kitaifa huenda zikaangazia vipimo laini kidogo vya kusaidia ujumuishaji wa bidhaa katika soko. Hii ni pamoja na ujumuishaji wa vifaa vya kusaidia mzunguko mfupi wa utoaji wa chakula ambavyo vinapatikana kwa wakulima na biashara ndogo ndogo zinazohusiana nazo katika muungano wa Uropa. Mapendekezo haya yanaingiliana na hitimisho ya ripoti ya EU kuhusu maeneo ya mashambani Afrika yanayohimiza mahusiano kati ya miji na vijiji kama sehemu ya mbinu ya kimaeneo ya mfumo wa chakula.

Kuongezea kwa mapendekezo haya, washika dau kutoka viwango mbalimbali vya kiutawala katika maeneo ya Afrika yaliyofanyiwa utafiti na SALSA, walitilia mkazo maeneo 5 yenye uhitaji kwa wakulima wadogo na wakapendekeza suluhisho sawa kwa mahitaji hayo.

Kutoka na miundo tofauti ya sera yanayotawala kila nchi na mipango ya vyama vya kimataifa vya pamoja, mapendekezo yanayooana na suluhisho hurejelea njia nzuri za aina kutoka kwa kila nchi na kuwaachia waamuzi kuangalia jinsi kila moja wa sera za kiserikali zinaweza kusaidi vipimo hivi.

©FAO/Roberto Faidutti

1) Vijana katika kilimo

Kuhusisha vijana katika kilimo ni muhumu kwa maendeleo ya jamii katika vijiji lakini ni wazi kwamba hakuna uhuinano kati ya elimu ya vijana na mazoezi katika sekta ya kilimo. Kuongezea kuna vikwazo mahususi yanayofanya vijana kutokuwa wakulima watajika. Vikwazo hizo ni;

- Ugumu wa kupata mikopo ya mashamba
- Fursa chache ya kupata kushiriki katika muundo wa sera
- Kukosa fursa ya kupendeza kama ya teknolojia mpya katika kilimo ama usaidizi wa uvumbuzi katika kilimo

Kilimo hakipigiwi debe kwa vijana kama Sanaa na biashara ya kuvutia!

Mabadiliko yanatakikana haswa katika utengenezaji wa sera, ubadilishaji wa teknolojia na uvumbuzi. Vijana huwa hawapati nafasi ya kuhususishwa katika uundaji wa sera za kilimo ambazo huwaathiri na hii huchangia katika sera ambazo hazijibu mahitaji yao. Mashirika ya vijana wa vijijini zingepaswa kuhusishwa na muundo wa mipango mpya ya kilimo.

Vijana huvutiwa na uvumbuzi wa kiteknolojia na kisosiolojia katika kilimo lakini hakuna usaidizi wa kutosha kwa uvumbuzi wa vijana na ujasiriamali. Utafiti katika kilimo huwa haishughulikii haja na matamanio ya wakulima wadogo.

Pesa za msaada zinahitajika ili kusaidia uvumbuzi wa vijana na ujasiriamali katika sekta ya kilimo ili kutambua na kutimia nafasi ya biashara ya wakulima wadogo, sana sana katika kuunganisha maeneo ya mjini na vijijini. Pasi na hayo, uvumbuzi kutoka kwa vijana wajasiriamali katika kilimo unapaswa kushirikishwa katika mfumo wa chakula wa kijijini ili kuhakikisha matokeo mazuri ya biashara hizi katika masoko ya kimitaa.

Mifano michache ya sera na mipango mizuri yaliyoangaziwa na washika dau kutoka kwa maeneo yalifanyiwa utafit na SALSA ni:

- Katika nchi ya Kenya kuna hatua na sera yanayosaidia vijana katika uvumbuzi. (mafunzo, kujifuza kutoka kwa watu wanaofanya shughuli sawa, ufadhili na kadhalika) haya yanalenga kufanya ukulima kuwa ya kuvutia zaidi kwa vijana na kuendeleza utendaji na sanaa katika biashara kupitia kufunzwa vizuri na tajriba.

- Sera ya maendeleo ya vijana ya kitaifa nchini Kenya (2018) inalenga kuwawezesha vijana kuchangia katika maendeleo kwa kubadilisha kilimo na kilimo biashara ili zivutie vijana. Kazi za muda za Vyuo vya teknolojia na mafunzo ya ufundi (TVET) yanatolewa kwa vijana nchini Kenya na kupita vyuo vya kilimo nchini Ghana.

- Nchini Ghana baraza la vijana la kitaifa lina jukumu la kushughulikia masuala ya vijana lakini hayajaweza kuhusisha vijana wote. Kuna vipindi vya vijana katika kilimo lakini vinaendeshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali mfano UWEZO nchini Kenya na kulima kwachakula na kazi nchini Ghana.

2) Upatikanaji wa mikopo nafuu

Mashamba madogo katoka maeneo ya SALSA huwa na ugumu katika kupata mikopo yenye nafuu katika kilimo kwa ajili ya pembejeo katika kilimo, vifaa na vingine. Taasisi za huduma za fedha zilizoko huwa hazitilii mkazo mahitaji ya mikopo kwa wakulima wadogo. Pia hazina bima kwa mazao ikiwa mazao hayatafanya vyema katika mazingira magumu yenye mabadiliko mengi katika hali ya anga.

Katika nchi nyingi barani Afrika yaliyofanyiwa utafiti na SALSA kuondolewa kwa vizungiti vya kijamii kama vile umri na jinsia ili kupata mikopo kutasaidia mashamba madogo pakubwa sana. Teknolojia ya kisasa ya ICT na mikopo ya kuwezesha kutumia runununu vimetambulika na washikadau wa SALSA kuwa na athari chanya kwa wakulima wadogo wa sehemu za vijijini lakini kuna wasiwasi kuhusu wakulima hao kuchangia kwa kuwa na madeni.

Maitafa mengi ya SALSA barani Africa (Ghana , Malawi na Tunisia) hutoa ruzuku katika bembejeo. Hata hivyo mipango hizi zinahimiza ukulima wa bembejeo kutoka nje. Kuna wasiwasi kuhusu madhara katika mazingira. Maamuzi kuhusu aina hii ya msaada unapaswa kuangaliwa kwa kina kwa kutilia maanani ushahidi wa kutosha na kujitegemea kutoka kwa mfumo wowote wa kisiasa

© SALSA

3) Mali asili na hali ya hewa

Njia tatu muhimu zilitambuliwa na washikadau wa SALSA kuhusu mali asilia na hali ya hewa barani Afrika.

- Huduma za kilimo ni muhimu katika kuelimisha wakulima na utawala wa kimitaa kuhusu mabadiliko katika hali ya hewa na madhara pamoja na kupata suluhisho.

- Mifumo ya kunyunyiza maji yanaweza kusaidia wakulima kuepukana na njaa.

- Mipango mahususi yanahitajika ili kupunguza ukataji wa miti ili kupata kuni.

Nchini Ghana na Kenya, mabadiliko katika sheria yamewezesha wanawake kumiliki na kurithi mashamba. Hii inaonekana kusaidia maendeleo endelevu katika uongozi wa mashamba.

Kenya imeanzisha mipango mengine ambayo yanasaidia maendeleo endelevu katika usimamizi wa mali asili na jinsi ya kukabiliana na mabadiliko kaika hali ya hewa kamavile mifumo gatuzi ya fedha kuhusu hali ya hewa. Mifano mengine yaliyofaulu ni pamoja na kuanzisha mradi safi wa kilimo na uhifadhi wa misitu nchini Ghana.

Pasi na kuwa na mifano mwafaka wa kuingilia kati kuna mawanda ya uboreshaji. Mambo muhimu ya kuangazia ni:

- Kukosa pesa za ufadhili ya usimamizi wa mali asili na mabadiliko ya hali ya hewa.

- Utegemezi katika misaada kutoka nje ama miradi yasiyofadhiliwa na serikali na miradi yenye kuzingatia sehemu chache na muda.

- Kukosa miradi yenye ushahidi katika miundo yao.

Washika dau wa SALSA nchini Kenya wametambua kwamba baadhi ya sera na mipango yanayokabili maendeleo endelevu katika usimamizi wa mali asili na kuhifadhi kilimo hayazingatiwi kuwa haja muhimu kwa mashamba madogo.Mfano ni njia zao za kufanya kazi. Kuelewa kwa undani kwa uchumi wa mashamba madogo ni kwa kuwezesha warsha na kuhusisha mashirika ya wakulima wadogo katika mipango ya uundaji ili kuhakikisha mwingiliano mzuri.

Huku miradi zinazoshughulikia usimamizi wa mali asili na mabadiliko ya hali ya anga yanafadhiliwa na mashirika ya nje ya Kenya (kama mashirika ya kimataifa ya maendeleo, wafadhili wa nje na mashirika yasiyo ya kiserikali) kuna tishio la kukosa kuendelea. Hata ingawa mipango haya yanaonyesha miigo yaliyofailu, wao hung'ang'ana kuonyesha matokeo yao kwa kuangazia eneo kubwa kuafikia maendeleo endelevu na kuwa wa kujitegemea. Mipango kama haya yanapaswa kuunda njia za kuondoka na kuhakikisha kuwa mashirika ya kiserikali yana uwezo wa kifedha na kikazi na pia kisiasa ili kutekeleza mipango.

4) bidhaa, soko na utangazaji wa bidhaa

Sehemu za kuingilia kati katika sera zilizonyeshwa na washikadau wa SALSA barani Afrika zilikuwa kuunda a) vitengo vya kutengeneza na kuhifadhi ili kuongeza dhamana kwa bidhaa kutoka kwa mashamba madogo na b) mifumo yaliyo na mwelekeo (kama jukwaa ya washikadau wa nje na mifumo ya kudhibiti bei) hii ni mahususi kwa wakulima wadogo wenye ujasiriamali.

Maendeleo yaliyoonekana katika miaka za hivi karibuni yamekuwa kuongezeka kwa upatikanaji wa taarifa kuhusiana na soko (kutegemea miktadha ya kitaifa) kupitia idhaa mbalimbali. Mikakati haya yanaathari nzuri kwa kusaidia wakulima kuelewa soko zaohivyo izidi kuimarishwa.

Masuala mengine yaliyoangaziwa na washikadau kutoka maeneo ya Afrika yaliyofanyiwa utafiti na SALSA ni:

- Pembejeo nyingi za ukulima ambazo wakulima wadogo hununua nchini Kenya huwa ghushi. Maendeleo na utekelezaji wa sheria ya kutathmini ama kuzuia mbolea na dawa za wadudu yachukuliwe kwa makini na serikali.

- Washikadau kutoka Kenya na Malawi waliripoti viwango vya vyakula vya nyumbani kutokana na wakulima wengi wadogo lakini wakaona kuwa uzalishaji wa kiwango cha chini ulizuia kuingia katika soko za kimaeneo. Wanasera wanahimizwa kutilia maanani vikwazo kwa uzalishaji wa mashamba madogo. Kuwepo kwa vifaa bora vya ukulima kutasaidia pakubwa kama pia yataandamana na maafisa wa kilimo watakaowafunza jinsi ya kutumia vifaa hivyo.

- Kuwepo kwa vyama vya pamoja ambavyo havifanyi kazi katika maeneo mengine yalionekana nchini Kenyana Malawi. Haya yanapatika katika miktadha fulani. Mahali kunakopatikana na shida hii huwa ni kizingiti kikubwa sana kwa kuingia kwa mashamba madogo katika soko za kitaifa na kimataifa. Katika kesi nyingi vidhibiti hupatikana tayari katika kusaidia ukuaji na ukusanyaji wa mifumo ya mashirika ya wakulima wadogo lakini hayatekelezwi kisawasawa katika viwango vya kijijini/kimaeneo.

  Uelewa wa ndani unahitajika kuhusu a) sababu za vyama vya pamoja kukosa kufanya kazi kikamilifu b) hatua gani inaweza kuchukuliwa ili kuepuka haya kwa mfano imependekezwa kuwa mikakati mahususi yanahitajika ili kuhakikisha kuingizwa kwa wakulima wachanga na wajasiriamali katika nafasi za uongozi wa vyama hivi vya pamoja.

- Ingawa ilionekana kwamba mashamba madogo hufaidi kwa soko zisizo na vikwazo na yenye mahitaji ya juu ya mazao kutoka kwao (kwa chakula lakini mazao ya kuuza kama chai, kahawa na koko.) baadhi ya wadau walisema kuwa kuwe na soko zilizo na muundo Fulani ambazo zitaruhusu wakulima wanaoweka mikataba. Hii itasaidia kutoa utabiri kwa wingi na kupunguza hasara kwa mashamba madogo. Kueleweka kwa kina wa ni nani waamuzi wa kimaeneo na kazi yao katika kila mkoa kutasaidia mashamba madogo.

5) Miundo misingi bora na uunganishaji

Ili kuimarisha uunganishaji na miundo misingi, sera za kuingilia kati zilizotambuliwa ni:

- Kuchukua tathmini zinazohitajika vizuri katika maeneo ya vijijini. Masuala kama ya upatikanaji wa umeme kwa bei ya chini lazima yaangaliwe tena; Uundaji na utunzaji wa barabara nzuri ili kuimarisha upatikanaji kwa soko.

- Utoaji wa rununu yenye udhabiti na kuunganishwa kwa mtandao. Kuwepo kwa mtandao mzuri wa rununu katika maeneo ya vijijini kutasaidia wakulima kutuma ujumbe kupitia mfumo wa ujumbe mfupi na sauti katika lugha asilia. Hii pia inaweza kukuza idhaa za redio na televisheni yanayotangaza habari kuhusu soko kwa wakulima kupitia lugha zao za kwanza.

- Miundo misingi bora ya unyunyizaji wa maji. Miundo misingi mikubwa huwa mradi unaondelezwa na serikali na yanaweza kutumiwa vibaya kwa sababu ya changamoto katika kiwango cha kuagizia. Mipango midogo ya unyunyizaji wa maji na yale makubwa ni muhimu sana kwa mashamba madogo.

MAPENDEKEZO YA DIOLOJIA YA EU-AFR NA MIPANGO YA PAMOJA

Ushirikiano sawa

Utafiti wa baadaye utakaofadhiliwa na Horizon Europe yaweke viwango sawa katika uwakilishaji wa washirika wa EU na AFR ili kuhakikisha kwamba upande wote una viwango sawa katika utendakazi katika miradi yote (hata miundo mahususi ya utafiti)

Kuendelea kusaidia utafiti wa kibara

Miradi ya SALSA yameonyesha utafiti wa mfumo wa kilimo na chakula katika bara tofauti. Utafiti ukifanyanywa Uropa na Afrika unazalisha maono muhimu na elimu katika bara zote. Masuala kutoka Uropa ni muhimu kwa washirika wa Afrika kwasababu nchi zao zinakua sana. Kuelewa kwa nguvu na udhaifu wa sera za kilimo barani Uropa(na athari yake kwa mashamba madogo) yanaweza kusaidia katika kufanya maamuzi. Washirika kutoka Uropa wanaweza kujifunza kutoka Afrika kuhusu njia zisizorasmi za kijamii ya kusaidia chakula na usalama wa lishe bora. Hivyo kufadhili utafiti wa bara tofauti kupitia kwa njia sawa ya ushirika katika utafiti lipewe kipa umbele.

Kusaidia utafiti wa kimaeneo na kuendeleza vyama vya ushirika

Washirika na wadau wa SALSA walisistiza haja ya kusaidia ushirika wa lugha katika utafiti na uvumbuzi (Nchi za Afika zinazozungumza Kireno, Kifaransa ama Kingereza) na njia za kimaeneo katika bara (mfano Uropa Kusini na Kaskazini) jukwa ya kimalengo yalianzishwa ili kusaidia kusemezana baina ya watafiti wa Afrika na Uropa.

Uwezo wa kubadilika katika mikataba

Uwezo wa kubadilika katika vidhibiti vya mikataba chini ya mpango wa Horizon 2020 ili kuonyesha utofauti katika usimamizi na mifumo ya kisheria za nchi husika kutasaidia kuwekwa kwa njia sawa katika miktadha tofauti na kupunguza pesa za huduma katika ushirika wa kibara.

Mwisho, kuweka pamoja mada za utafiti ambapo washirika katika utafiti wa AFR watajumuishwa katika njia ya kuwa na ushirika wa utafiti na uvumbuzi uliofadhiliwa pamoja wa EU-AFR kuhusu chakula na usalama wa lishe na maendeleo endelevu katika kilimo yayoweza kusaidia uhuiano wa kazi za utafiti kutoka kwa washirika wote.

MAPENDEKEZO KWA SERIKALI NA WASHIRIKA KATIKA MAENDELEO YA AFRIKA WANAOUNGA MKONO SERA ZAO KUHUSU KILIMO NA USALAMA WA CHAKULA NA MIPANGO

Kutambua utofauti wa mashamba na bishara ndogo ndogo katika sera ya kilimo na chakula

Ingawa harakati ya CAADP inawezesha nchi kutumia nguzo zake katika miktadha za kitaifa, mifumo ya chakula na kilimo ya nchi nyingi barani Afrika hayatofautishi moja kwa moja kati ya mashamba tofauti Mahitaji (utendakazi na usaidizi) ya mashamba yenye kiasi tofauti na uingiaji katika soko ni tofauti. Haya ni lazima yajitokeze katika sera zote. Aina ya kitaifa yenye ushahidi ni muhimu.

Kutambua kwamba ukulima wa muda unaweza kuwa chaguo hivyo unahitaji usaidizi

Huku ukulima wa muda ni kawaida kwa mashamba madogo barani Afika na Uropa hakuna utambuzi wa njia hii na usaidi wowote kwayo.Mfumo wa msaada kama vile DIFD'S Conceptual Framework on Agriculture yanaweka mambo matatu kwa wakulima 'kuenda juu' (kuimarika kwa kilimo na uingiaji katika soko), 'kwenda chini'(kuacha kilimo kwa wafanyakazi wasio wakulima) ama 'kubakia hapo'(mipango yasiyoendelevu)

Hata hivyo, kusaidia wakulima wadogo wa muda kwa mchango wao kwa usalama wa chakula na lishe kando na kuendeleza kazi vijijini inaweza kuwa njia mwafaka inayohitaji usaidizi.

© SALSA

salsa
small farms
small food businesses and
sustainable food security

Mawasiliano:

www.salsa.uevora.pt/en/

www.fao.org/in-action/small-farms-businesses-sustainable-food-nutrition

@SalsaH2020 *Tufuate!*

Tegea: Teresa Pinto-Correia, Universidade de Évora, Portugal mtpc@uevora.pt

Warsha ya mwisho ya SALSA → katika warsha ya 14 IFSA 2020
Évora, Ureno

Mradi huu umepata ufadhili kutoka kwa muungano wa Uropa EU Horizon 2020, mpango wa utafiti na uvumbuzi kwa mkataba wa nambari 677363